# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
# SHULE YA SEKONDARI CHANZURU
# S.L.P. 179, KILOSA

**Kumb. Na: CHSS/JI/F.I/ 2020**

**JINA LA MWANAFUNZI ..........................................................................................**

**............................................................................**

**YAH: KUJIUNGA NA SHULE HII KIDATO CHA KWANZA (1) –**

1.0 **UTANGULIZI:**

Napenda kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Chanzuru kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo **2021** Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/01/2021**

2.0 **MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 **SARE ZA SHULE**

2.1 **A: WASICHANA**

(i) Seti za kijivu mbili (inayogusa soksi, marinda sita, belt dogo inayovaliwa tumboni)
(ii) Shati nyeupe ndefu za miko mifupi mbili (aina ya Tomato)
(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu.
(iv) Soksi nyeupe jozi/pea mbili
(v) Sweta la bluu
(vi) Hijabu ndefu na nusu kanzu kwa wanafunzi wa kike wa kiislam

2.1 **B: WAVULANA**

(i) Suruali za kijivu mbili, upana chini iwe 17 cm, yenye marinda mawili kila upande, turn up isiwe na mifuko ya jinsi. Iwe na luxi.
(ii) Shati nyeupe za mikono mifupi mbili (aina ya Tomato) iwe ndefu inayoweza kuchomekewa.
(iii) Viatu vyeusi vya ngozi na vya kamba.
(iv) Soksi nyeusi jozi/pea mbili
(v) Sweta la bluu.
(vi) Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi usio na urembo wala mpana zaidi ya sentimita tatu.
(vii) T.Shirt ya kijani.

2.2 **VIFAA VYA DARASANI**

(i) Daftari kubwa (Counter book quire Two) kumi (10)
(ii) Begi la kuhifadhia vifaa vya darasani (Begi la mgongoni) lenye uwezo wa kubeba madaftari yote kumi.
(iii) Mkebe, kalamu za wino (bluu na nyeusi), kalamu za risasi, graph pad na rula.
(iv) Vitabu vya kidato cha kwanza kwa wenye uwezo: mfano Kamusi ya Kiingereza.

Scanned with CamScanner

2.3 **VIFAA VYA USAFI**

(i) Ndoo ndogo moja ya lita kumi (10)
(ii) Fagio la chelewa moja
(iii) Fyekeo au reki moja (1)

2.4 **SARE ZA MICHEZO**

(i) T-Shirt ya kijivu kwa wasichana na wavulana
(ii) Bukta ya bluu kwa wavulana na sketi ya bluu kwa wasichana
(iii) Viatu vya michezo (Raba za michezo) aina ya njumu.

**NB:** MWANAFUNZI ATAPOKELEWA ENDAPO TU ATAFUATA TARATIBU NA MAELEKEZO YOTE YA KUJIUNGA NA SHULE IKIWA NI PAMOJA NA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA NA KUJAZA FOMU YA TAARIFA ZA AFYA (MEDICAL EXAMINATION).

3.0 **SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya ELimu Na. 25 ya mwaka 1978 inayozingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Sheria zote za shule zimewekwa ili kuwawezesha wanafunzi kulifikia lengo la kuwapo kwao hapa shuleni bila matatizo. Aidha sote tunaelewa kuwa nidhamu nzuri huambatana na mafanikio mazuri kitaaluma pia. Hivyo utatakiwa:

- Kuwepo ndani ya mipaka ya shule muda wote wa masomo na kazi.
- Kuhudhuria vipindi vyote vya shule darasani na nje ya darasa, ifahamike kuwa kutoroka vipindi au shuleni ni kosa kubwa.
- Kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote wakiwemo walimu wanapoingia darasani na maeneo mengine makubwa watakapokuwapo.
- Kutotumia lugha mbaya wakati wote kati yako na wanafunzi wengine au kwa walimu na kwa watu wengine.
- Kutovaa vidani kama vile hereni,mikufu, bangili, kutotia dawa nywele.
- Kutojichora kwa hina au tatoo sehemu ya mwili wako.
- Ni lazima kusimama mwalimu aingiapo darasani na kusalimia.
- Kutotembelea nyumba za kulala wageni na kumbi za starehe.
- Kutokuwa na kucha ndefu na kutopaka rangi au hina.
- Wasichana wanatakiwa kukata nywele nusu inchi.
- Wavulana hawaruhusiwi kufuga ndevu wala nywele ndefu, nywele zikate nusu inchi. Lugha chafu na matusi ni marufuku.
- Kuvaa sare ya shule muda wote wakati wa masomo darasani, nje ya shule kwa shughuli za kishule.
- Kutokuwa na simu ya mkononi, SIM CARD au vicha awapo shuleni.
- Kutovaa kofia, jaketi, sweta ambalo siyo la shule.
- Kufanya usafi binafsi na wa shule, mazingira na darasani.
- Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
- Kutovaa nguo za mitindo ya LEGEZA na mitindo mingine ya kihuni.
- Kutokwenda nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalumu.
- Mafuta yenye harufu kali hayaruhusiwi.
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.
- Kuheshimu bendera na wimbo wa Taifa.

Scanned with CamScanner

- Kutoandika katika vitabu vya shule, kuta, madawati, viti na ubao wa kufundishia.
- Kufanya biashara ya aina yoyote katika eneo la shule.

**TANBIHI**

(i) Adhabu kali zitatolewa kwa wanafunzi wote watakaokiuka sheria za shule.

(ii) Simu, nguo za nyumbani na vitu vingine visivyotakiwa shuleni vitachukuliwa na havitarudishwa, vyote vitaharibiwa mbele ya wanafunzi wengine.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati, ukabaji, usagoga na ulawiti
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yoyote ya kulevya.
4. Makosa ya jinai
5. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzako, mwalimu au mtumishi asiye mwlaimu.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.
7. Kudharau bendera na wimbo wa Taifa.
8. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
9. Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
10. Kuoa au kuolewa
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
12. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu.
13. Utoro (kukaa nje ya shule bila taarifa kwa zaidi ya siku 90).
14. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani shuleni.
15. Kukutwa/kuwa na simu ya mkononi, SIM CARD au vicha shuleni.
16. Kutembelea nyumba za kulala wageni, kumbi za starehe, baa, klabu na sehemu nyingine ambazo kisheria mwanafunzi haruhusiwi.
17. Kucheza kamali: mfano pool table nk.

## 4.0 MWISHO

Nachukua nafasi hii kukukaribisha shule ya Sekondari Chanzuru na ni matarajio yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyopewa na Taifa lako.

..............................

**REHEMA J MKWAY**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI CHANZURU
S.L.P. 179-KILOSA

Scanned with CamScanner